# JARIDA LA RHRP

Habari! Karibu kwenye toleo la kwanza la Jarida la program ya Afya ya Uzazi na Mahusiano ya Empower Tanzania. Jarida hili litatolewa kila mwezi ili kukupa taarifa za maendeleo ya programu, kutoa maelezo ya ziada pamoja na mengineyo machache.

## NINI KIPYA?

Umekuwa mwanzo wenye kazi kubwa katika program ya Afya ya Uzazi na Mahusiano. Tangu sisi wote tulivyokutana mwezi wa tisa mwaka jana ,walimu 177 wa shule za msingi na walimu 264 wa shule za sekondari (ikiwa ni pamoja na ToTs) wamepokea mafunzo katika shule 19 za wilaya ya Same. Hii ni NZURI sana.

Zaidi ya hayo, tumekamilisha upimaji wa awali wa wanafunzi. Hii inatupa msingi wa kulinganisha tutakaporudia majaribio mwishoni mwa mwaka. Wafanyakazi wa Empower Tanzania wamekuwa na kazi ngumu yakuingiza data zote katika sahajedwali. sahajedwali hizo hutumwa kwa statistician na mtafiti huko marekani (John Peden na Joanne Chopek-Foss) ambao watachambua namba hizo na kutoa ripoti.

Wafanyakazi wa Empower Tanzania wamekuwa pia wakifanya kazi kubwa kutafuta fedha ili kuendeleza programu hii baada ya mwaka wa kwanza kupita. Hadi sasa, tuna matumaini chanya ingawa kazi kubwa zaidi inahitajika.

Sisi sote tunafanya kazi kwa pamoja ili kutengeneza timu yenye nguvu!



## Uangalizi:

Tunataka kujua kuhusu wewe!

Tungependa kuongeza sehemu ya uangalizi ya mtu kila mwezi - tutumie taarifa zako unazofundisha kipindi taarifa chache za kwako binafsi—unaweza ukajiona mwenyewe hapa katika toleo linalofata.

# MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA:

Sehemu hii imeundwa ili kujibu baadhi ya maswali tuliyopata juu ya programu

**Q: Nimekuwa nikiiulizwa swali la afya ya uzazi ambalo siwezi kulijibu, nifanye nini?**

A: Hakuna mtu anayeweza kujua kila kitu! Tuko hapa kusaidia na kusaidiana na kuwa na mtandao mkubwa wa wataalamu ambao tunaweza kupata majibu kutoka kwa madaktari, wauguzi, washauri na viongozi wa dini. Wasiliana na sisi na tutakupa jibu. Ruhusu vijana kujua kwamba utapata majibu, na uhakikishe kuwa utayajibu kipindi kinachofata mtakapokutana.

**Q: Je! Mwalimu wa kiume anaweza kufundisha kuhusu bidhaa za hedhi?**

A: Bila shaka. Jiweke huru na bidhaa kabla ya kipindi na fanya utafiti wa jinsi ya kutumia na kufua pedi. Hata hivyo, tunaelewa baadhi ya walimu wanaweza wasijisikie vizuri/huru kwa mara ya kwanza. Ikiwa hii inakuhusu wewe, unaweza kuwa na mwalimu wa kike pamoja na wewe katika kipindi kukusaidia kufundisha wanafunzi habari hii muhimu. Unaweza kujifunza kwa njia hii pia!

**Q: Ninapata shida kukabiliana na hisia zangu kuhusu unyanyasaji wa mtoto, Je nifanye nini?**

A: Ni kawaida kabisa kujisikia huruma kwa ajili ya mtoto na hasira kwa wahalifu. Ingawa, ni muhimu sana kujiangalia. Ongea na sisi, ikiwa hatutaweza kukusaidia, tunaweza kukusikiliza na kukupa mawasiliano ya mtu ambaye anaweza kukupa ushauri. Kujadili hali husaidia. Jaribu kuwashirikisha mawazo yako wenzako – huenda wengi wanahisia sawa na wewe. Pia ni muhimu kutafuta vitu vya kufanya ambavyo vitakusaidia kuwa sawa, inaweza kuwa kusikiliza muziki, kutembea au shughuli nyingine. Ikiwa bado unapata shida, tafadhali usisite kuwasiliana na sisi.

# SEHEMU YA KUZINGATIA:

Tunataka kujikita katika mada moja katika kila toleo ili kutoa maelezo ya ziada. Hii itachaguliwa bila utaratibu, lakini kama una ombi, Tafathali wasiliana na Jessica!



# MAELEZO KUTOKA KWA DR. JEFF:

Tuna furaha sana kuhusiana na kazi yako katika programu ya Afya ya Uzazi na Mahusiano (RHRP). Kama unavyojua, elimu hii itawafundisha vijana ujuzi muhimu wa uhusiano na taarifa sahihi kuhusu ngono. Kuondoa hadithi nyingi za ngono ni sehemu ya mchakato wa elimu hii, hivyo usiwe na aibu juu ya kuuliza maswali. Wafanyakazi wetu wanaweza kukusaidia kutafuta majibu ya maswali ambayo hauna uhakika nayo. Tipigie tu simu au tuma barua pepe au ujumbe wa maandishi.

Tafadhali panua kazi yako zaidi ya wanafunzi ijumuishe wazazi na wanajamii wengine. Elimu unayotoa inaweza kubadilisha maisha na jamii. Kila mtu anatakiwa kujua kuwa elimu ya afya ya uzazi imeonyeshwa kwa:

>Kupunguza mimba za utotoni
>Kupunguza magonjwa ya ngono
>Kuchelewesha muda wa kujiingiza kwenye masuala ya ngono kwa vijana

Wazazi pia wanapaswa kuelewa kuwa kufundisha vijana kuhusu afya ya uzazi imeonyeshwa kuwafanya vijana KUPUNGUZA kufanya ngono, na sio kufanya ngono zaidi.

Kama walimu, mna athari kubwa katika maisha na hatima ya wanafunzi wako. Kazi yetu ni kuiwezesha kazi yako muhimu. Tafadhali tujulishe jinsi gani tunavyoweza kusaidia!

# PROGRAMU NYINGINE ZA EMPOWER TANZANIA

Katika sehemu hii, tunataka kukujulisha juu ya kazi nyingine ambazo Empower Tanzania inafanya. Sasa wewe ni sehemu ya kitu kikubwa zaidi.

Pedi za kufua (RMKs) ni aina ya bidhaa za usafi za wanawake ambazo zinaweza kutumika kama mbadala wa pedi za kutupa. Pedi za kufua zenye gharama nafuu zinajumuisha pedi na kizuizi cha unyevu ambacho kinamlinda msichana katika katika mzunguko mzima wa hedhi na hufuliwa kwa ajili ya maandalizi ya mzunguko unaofuata. Kwa kipindi cha miaka mingi wanawake na wasichana mara nyingi wamekuwa wakitumia kitambaa cha nguo zilizochakaa (vitambaa) ili kushika damu yao ya hedhi. Shirika la Empower Tanzania, kwa kushirikiana na Days for Girls, imefundisha vikundi 10 ambavyo ni waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia (GBV) kushona pedi za kufua, ambazo huuzwa kwa wanawake na wasichana katika Wilaya ya Same na mikoa ya karibu.

Pedi hizi hujumuisha vizuizi viwili vya unyevu, vitambaa 8 laini vya pamba, mfuko wa plastiki kwa ajili ya pedi zilizotumika na mfuko wa kitambaa wa kubebea pedi. Zinaweza kufuliwa kwa mkono na kuanikwa juani na kwa kawaida hudumu kwa miaka 3. Vikundi 10 ya GBV hutengeneza pedi na waelimishaji 33 wa Afya huziuza bidhaa hizi kwa jamii. Pia hutoa elimu ya afya ili kuongeza ufahamu juu ya hedhi ambayo bado inachukuliwa kuwa ni mada mwiko kuzungumzia. Pedi za kufua zitawawezesha wasichana kuendelea na masomo kwa heshima na ujasiri.

## Uangalizi:

Tunataka kujua kuhusu wewe!

Tungependa kuongeza sehemu ya uangalizi ya mtu kila mwezi - tutumie taarifa zako unazofundisha kipindi taarifa chache za kwako binafsi— unaweza ukajiona mwenyewe hapa katika toleo linalofata.

## Sasa wewe ni sehemu ya kitu kikubwa zaidi.



# KUTANA NA TIMU

Katika sehemu hii ya jarida, tungependa kuwatambulisha timu yetu, mtu mmoja kwa wakati mmoja. toleo hili litamtambulisha Catherine Wales, kiongozi wa program ya RHRP.



## CATHERINE JOHN WALES

Mratibu wa Miradi ya Afya

Jina langu ni Catherine John Wales. Nimekuwa nikifanya kazi na shirika la Empower Tanzania tangu Mei 2017 kama Mratibu wa Programu za Afya. Pia ninafanya kazi kama Meneja wa Programu ya Afya ya Uzazi na Mahusiano. Nina shahada ya maendeleo vijijini kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), pia nina stashahada ya mipango ya maendeleo na astashahada ya mipango ya maendeleo vijijini kutoka Taasisi ya Mipango ya Maendeleo Vijijini. (Mipango) Hapo awali nilifanya kazi na shirika la Word Vision Tanzania katika mradi wa Maisha stahimilivu.

Nia yangu kuu ni kufanya kazi na jamii zenye uhitaji-hasa makundi yaliyotengwa/sahaulika — kusaidia, kuunga mkono, na kutafuta suluhisho kwa pamoja la shida na matatizo yao makuu.

## WASILIANA NASI:

Ikiwa una maoni au mapendekezo juu ya jarida hili tafadhali tuma barua pepe kwa Jessica katika jhaw1@gmail.com yenye kichwa cha habari "jarida". Ikiwa unahitaji msaada wowote unaohusiana na masuala ya kufundisha tafadhali wasiliana na Catherine katika catherinewales17@gmail.com au Yoeza katika yoeza1mnzava@gmail.com

ETI EMPOWER TANZANIA